

Umoja wa Mataifa

Ushirikiano kati ya Benki ya Dunia na [UN \[Umoja wa Mataifa\]](#) umekuwepo tangu kuanzishwa kwa mashirika haya mawili (1944 na 1945) na hushughulika na maswala ya kiuchumi na kijamii kama vile kupunguza umasikini, kuchangia maendeleo ya kudumu, na uwekezaji katika watu. Mbali na kuwa na ajenda yapamoja, Benki na Umoja wa Mataifa wana wanachama waliosawa, na ni nchi chache tu ambazo ikiwemo Cuba na Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Korea, sio wanachama wa Benki.

Uhusiano rasmi wa Benki na Umoja wa Mataifa unaelezwa na makubaliano ya 1947 yanayo tambua Benki kuwa shirika huru maalumu la UN pamoja na kuwa mwanachama na mkaguzi katika mashirika mengi ya UN. Uvumbuzi wa hivi karibuni unaonyesha kwamba namna ya ushirika kati ya mashirika haya mawili ya Umoja wa Mataifa na Bretton Woods ni thibitisho la kuwepo kwa uhusiano wa upana mkubwa na unaokuwa kati yao.

Benki pia ina uhusiano na UN katika kiwango cha kisiasa na cha uandalizi wa sera katika kazi za Baraza Kuu na kamati zake, [Economic and Social Council \(ECOSOC\) \[Baraza la Uchumi na Mambo ya Jamiil\]](#), ambalo wanachama wake walishiriki katika mazungumzo kuhusu maswala ya maendeleo pamoja na Wakurugenzi Watendaji wa Benki, na wa mashirika kama [United Nations System Chief Executives Board for Coordination \[Bodi za Usimamizi la Watendaji Wakuu wa Mfumo wa Umoja wa Mataifa\]](#). Ushirikiano huu wa mapana marefu katika kiwango cha kimataifa na cha nchi huwa ni pamoja na:

- Katika kiwango cha uendeshaji, Raisi wa Benki na Katibu Mkuu wanafanya mazungumzo ya kawaida kama kuangamiza umasikini, kuongezea Afrika uwezo wa kazi, maswala ya usaidizi baada ya vita, haki za binadamu, na udhamini wa maendeleo. Zaidi ya hayo, Rais Wolfensohn hushiriki kikamilifu katika mabaraza mbalimbali ya UN kama ECOSOC Substantive Session policy dialogue [Mashauri ya Sera ya Mapato ya ECOSOC], na pia hustawisha mazungumzo na viongozi wa Programu za UN, Mashirika Maalum na Kamati kama ile ya [High Commissioner for Human Rights \[Kamati ya Haki za Binadamu\]](#).
- Katika kiwango cha kisiasa, kama ilivyowakilishwa na nchi wanachama, Benki ina jukumu la kuwa mkaguzi katika mashirika kadhaa ya UN, ikiwemo: Baraza Kuu na Second and Third Committees [Kamati zake za Pili na Tatu] na ECOSOC, ambayo huangalia maswala ya mambo yanayofikiana na shughuli za Benki kwa mfano: ongezo la watu duniani, umasikiini, HIV/UKIMWI, maswala ya kijinsia na wanawake na maendeleo, shughuli za kiserikali na utumishi wa umma, mawasiliano, na mazingira. Bank pia hustawisha mazungumzo na nchi binafsi wanachama na makundi ya kisiasa kama vile G-77 na Jumuiya ya Ulaya.

Katika kiwango cha utendaji, Benki, ikiwa shirika maalum la UN hufanya kazi na [United Nations Development Programme \[Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa\]](#) na hazina na Programu nyengine za UN katika miradi yake kwa kupitia usimamizi wa sera, utekelezaji wa miradi, udhamini wa pamoja na usimamizi wa misaada. Kwa mfano, Benki ni mmoja wapo wa wafadhili sita washiriki wa Joint [United Nations Program on AIDS \(UNAIDS\) \[Programu ya Pamoja ya Umoja wa Mataifa ya UKIMWI\]](#) na mmoja wanao changia kwa wingi zaidi ulimwenguni katika vita dhidi ya HIV/UKIMWI. Na ushirikiano wa Benki na [World Food Program \(WFP\) \[Mpango wa Ulimwengu wa Chakula\]](#) hujumuisha miradi yao ya programu za chakula-kwa-kazi na miradi ya Benki ya ufwatilizi wa uwekezaji. Pia, Benki ni sehemu muhimu ya mpango wa Kimataifa wa Umoja wa Mataifa. Benki husaidia kuandaa na pia hushiriki katika mikutano karibu yote ya UN, na ikiwa mwanachama wa kundi la kufwatilia mikutano ya Umoja wa Mataifa, hutekeleza malengo ya Umoja wa Mataifa katika kiwango cha nchi.

Kwa mengi zaidi kuhusu Umoja wa Mataifa, anagalia [UN System of Organizations \[Mfumo wa Mashirika ya Umoja wa Mataifa\]](#).